# MKIA WA MBUZI

Motyani ni msichana anayependa sana kuhadithiwa hadithi mbalimbali. Anaishi na Bibi yake ambaye ni mzee. Kichwa cha nyanya yake kimejaa mvi nyeupe. Mara nyingi huwahadithia wajukuu zake na watoto jirani hadithi.

Siku moja usiku Motyani alimwambia Bibi yake amsimulie hadithi nzuri ambayo hajawahi kuisikia. Bibi yake akamjibu, "sawa lakini nimechoka nataka kwenda kulala." Lakini Motyani alimbembeleza ili amhadithie tu. Basi Bibi yake alikubali.

Akaanza kwa kusema, "hapo zamani katika nchi fulani aliishi Mzee mmoja aliyekuwa maskini mno. Hakuwa na mtoto hata mmoja kwa sababu wote walikufa kwa ugonjwa mbaya. Aliweza kufanya kazi kidogo katika shamba lake lililokuwa dogo. Hivyo kila mwaka alikuwa hana chakula cha kutosha. Hata wakati fulani njaa ilipoingia nchini mwao, Yeye alipata taabu sana. Alikula makombo katika nyumba za jirani. Pengine alilazimika kutafuta chakula jalalani. Hakuna hata mtu aliyemsaidia wala kumhurumia."

Alipofika hapo, Motyani akasema, "Bibi kwa nini watu wa nchi hiyo walikuwa wabaya hivyo?"

Bibi yake akajibu, "sikiliza kwanza, mbona una haraka?" Bibi akaendelea, "Mzee huyo aliishi katika hali hiyo kwa muda wote. Hata alipokuwa mgonjwa hakuna aliyempa msaada wowote. Mara chache chifu aliweza kutuma watumwa wake kumhudumia. Alifanya hivyo ikiwa alisikia wananchi wakilalamika.



Ama kweli mjukuu wangu duniani kuna dhiki na mateso." Bibi alimalizia usemi.

Motyani akabaki ameduwaa, huku macho yamemtoka kama gololi. Akamwambia Bibi yake, "kama ningeishi wakati huo ningemsaidia."

Bibi yake akamjibu, "pengine ungeweza Motyani. Lakini inataka moyo, kwa sababu wengi hushindwa."

"Ehe! endelea Bibi, hadithi hii inaleta huzuni sana." Motyani alisema.

Yule bibi aliendelea, "siku moja yule mzee alizunguka kutwa nzima kutafuta chakula mpaka nyumbani kwa chifu. Alipofika hapo, watumwa walimpa habari. "Yule mzee Maskini yupo na hali yake ni mbaya sana."

Yule chifu akasema, "mwondoeni haraka sitaki kusikia sauti yake wala kumwona hata sura kabisa."



Wale watumwa wakambeba juu juu kama gunia la mkaa. Ndipo yule Babu akalia kwa uchungu na kusema, "mkia wa mbuzi hufagia anapolala tu."

Motyani akasema, "bibi, nini maana ya maneno hayo?"

"Ingawa mbuzi anapenda kufagia sehemu kubwa ili ajipumzishe, lakini kutokana na ufupi wa mkia wake, hulazimika kufagia sehemu ndogo tu." Alisema bibi yake.

Motyani aliuliza tena huku machozi yakimlengalenga machoni, "sijaelewa bibi. Hebu nieleze zaidi."

Bibi yake akamwambia, "maskini hata kama atahitaji kitu zaidi, hawezi kupata isipokuwa atapata kidogo. Kwa hiyo hali yake itabaki vile vile."

Hapo Motyani tena akaanza kulia na kuomboleza. "Dunia hii ni mbaya bibi. Kwa nini hata watawala hawana huruma? Ingefaa wakuu wa namna hii washitakiwe katika mahakama za nchi zao."

Bibi yake akadakia, "nyamaza mjukuu wangu nikuleze mambo yaliyoko ulimwenguni humu. Watu wanakosa huruma kama vile dubu mwenye watoto. Hata hivyo leo utajifunza pia kutokana na hadithi hii."

Basi Motyani akafuta machozi. Macho yalimvimba yakawa mekundu kama amepaka pilipili. Hata uso ukavimba kwa ajili ya kilio kile.

Bibi akaendelea na hadithi, "Yule mzee alipofikishwa nyumbani kwake, alitupwa chini kama mzigo puu!"



"Maskini jamani," Motyani alisema na kuanza kulia tena.

"Nyamaza Motyani niendelee kukuhadithia basi." Alisema bibi yake.

"Alipoanguka chini, kumbe alitanguliza kichwa chini miguu juu. Shingo yake ikadididimia ndani na kuvunjika mikono yake yote. Kwa kuwa alikuwa mzee, hakuweza kustahimili vishindo vile. Kwa hiyo hakuweza kuishi tena akafa baada ya siku chache kupita."

"Mama weel" Motyani aliangua kilio.

Ndipo Bibi yake alimkumbatia na kujaribu kumtuliza lakini. Yeye aliendelea kulia na kujigalagaza kifuani mwa bibiye. Motyani alimhurumia sana babu yule. Bila shaka alimlinganisha na Babu yake aliyekuwa mzee pia. Alikuwa na huzuni kiasi cha kushindwa kutembea. Mwili ulichoka kama mtu aliyeshinda na kazi ya shamba.

Akamwambia, "je, Mjukuu wangu umejisikiaje baada ya kukusimulia hadithi ambayo hujawahi kuisikia?"

Motyani akamjibu, "leo nimejifunza sana bibi. Kweli inanilazimu kuwa na huruma kwa kila mtu."

Bibi yake akazidi kumweleza, "katika maisha yako mjukuu wangu, jihadhari sana. Uwe na upendo na kila mwanadamu. Usiwaonee watu wala kuwatesa kwa namna yoyote. Kumbuka nao walizaliwa kama wewe na kwamba wanataka rehema ya Mwenyezi Mungu. Ukiwa shuleni uwaheshimu walimu wako. Watoto wenzako uwapende kama unavyojipenda wewe. Unasikia Motyani?" Bibi yake alimaliza.

"Ndiyo Bibi si kusikia tu ila nimeelewa. Nimekosea hivyo mara nyingi katika maisha yangu bibi. Nimekuwa mkaidi sana kwa walimu shuleni hata kwa wanafunzi wenzangu pia. Nimewapiga wengine bila huruma sawasawa kabisa na chifu wa nchi ile. Nimekuwa mchoyo mno kwa sababu sikuwasaidia wenzangu walipopungukiwa na kitu fulani. Kwa hiyo bibi nakushukuru kwa hadithi hii. Nitakwenda kuwaomba msamaha wenzangu wote niliowakosea. Hata wewe naomba unisamehe kwa makosa yangu yote." Motyani alimaliza na kuanza kulia kwa nguvu.

Hatimaye Bibi yake akamnyamazisha. Wakaenda kulala. Ulikuwa ni usiku wa manane walipokwenda kupumzika.